



# Wafanyakazi wawasilisha kilio chao kwa waziri Mpina

Na Suleiman Abeid, Mwanza

■ ■ BAADHI ya wafanyakazi katika viwanda vya kuchakata minofu ya samaki wilayani Ilemela mkoani Mwanza wamelalamikia kitendo cha kufanya kazi katika mazingira mabovu yanayohatarisha afya zao huku wakilipwa mishahara kidogo. Hali hiyo imebainishwa jana na wafanyakazi wa kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki cha Victoria Perch Limited mbele ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi nchini, Luhaga Mpina aliyekuwa na ziara ya kufembelea baadhi ya viwanda vinavyochakata minofu ya samaki vilivyopo mjini Mwanza.

Wafanyakazi hao walisema, pamoja na kupata ajira katika kiwanda hicho, lakini wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira hatarishi kutokana na baadhi ya maeneo ya kazi kutokuwa na hewa ya kutosha hali inayowaathiri baadhi yao vitua na kwamba ipo hatari wengi wao watapoteza

maisha. Akifafanua mmoja wa wafanyakazi hao, Adamu Issa alisema wamekuwa wakufanya kazi katika mazingira mabovu kutokana na eneo la kufanya kazi kutokuwa na hewa rafiki kufya na kumtaka waziri afikire tofauti aliyopona yeye mwenyewe wakati akiwa nje ya kiwanda na baada ya kuingia kwandani.

"Nafiki waziri wewe mwenyewe umejironea, ulipokuwa pale nje palikuwa na hewa nzuri sana na uliponga hapa hewa imebadilika, sasa fikiria kama tunakaa humu ndani kati ya saa nane hadi tisa, je! hali zetu zinakuwaji?"

"Je? wafanyakazi tukiathirika kufya hvi viwanda vinavyohimzwa na Rais wetu Dkt. John Magufuli vitaaji watu gani, au mtakuwa mnakodi wafanyakazi kutoka China? Sisi tunamuunga mkono Rais wetu, lakini kama tukathirika kufya viwanda vitakavyojengwa vitapata wapi wafanyakazi, hapa kwetu wengi wetu vitua vimeisha kutokana na vitendea kazi vbovu

hasa hewa," alieleza Issa.

Pia wafanyakazi hao waliomba serikali iangalie kuhusu mishahara wanayolipwa baadhi ya watumishi walioajiriwa katika sekta binafsi kutokana na wengi waajiri kuwalipa wafanyakazi wao mishahara isiyokidhi matumizi yao ya mwezi mzima.

Kwa upande wao watumishi katika kiwanda cha uchakataji wa mabondo ya samaki cha Honglin International Trade Development Company Limited cha mjini Mwanza walimpongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi nchini, Luhaga Mpina kutokana na agizo lake la kupiga vita uvuvi haramu.

Wafanyakazi hao walimuomba Waziri Mpina aendelee kukaza nati na kutoruhusu kabisa uvuvi haramu ili pawepo na ongezeko kubwa la samaki katika maziwa ya hapa nchini hali itakayoweza wao kuendelea kupata ajira za uhakika.

"Mheshimiwa waziri kwanza tunakupongeza sana kutokana

na agizo lako la kuanzishwa operesheni sangara hapa nchi ukweli ni kwamba operesheni imeweza ongereko la samaki wengi na wenye viwango, hata ambayo imeweza viwango kuendelea kufanya kazi na kupata ajira.

"Tunakupongeza sana, endelea kukaza nati usiwegeze hata kidogo maana vinginevyo samaki wote wakitoweka kutokana na uvuvi haramu hata sisi marsha yetu yatakuwa hatarishi kutokana na kukosa ajira na familia zetu zitaathirika," alieleza mfanyakazi Shadia Shabib mwanamuziki mkuu wa wafanyakazi.

Akiibu malalamiko hayo Waziri Mpina alisema, aneyapokea atayafanya kazi kwa kuyafikishi kwa wanaohusika ambapo pengine alimwaga mkurugenzi wa huduma za uvuvi kutembelea kiwanda hicho ili kuweza kukagua miundombinu yote ya kufanya kazi na mazingira ya kufya na kwamba kazi hii itanyike ndani ya wiku moja.



# Lake Zone, Kigoma region plan new tourism and investment forum

From **SULEIMAN SHAGATA in Mwanza**

**L**AKE Zone and Kigoma Region plans a new Tourism and Investment Forum in Mwanza City to expose tourism opportunities found in the area so as to attract foreign and internal tourists to visit attractions found there.

Speaking to Region Administrative Secretaries (RAS) from Lake Zone and Kigoma Regions in Mwanza City over the weekend, the Permanent Secretary in the Ministry of Natural Resources and Tour-

ism, Prof Adolf Mkwinda emphasized on the need to speed up the process of establishing tourism and investment fair in the region.

He said that the agreement made early December this year to plan strategies and enable the envisioned Tourism Fair and Investment Forum to take place so as to expose some tourism attractions and opportunities found in Lake Zone and Kigoma Region they made agreement to speed up the process in order to present the idea to the regional commissioners and ministers for implementation.

Prof Mkwinda said that tourism is a sector which contributes a lot of money to the national coffers through the national parks, game reserves and forest reserves which are also found in the Lake Zone and Kigoma Regions but until now about 80 per cent of tourists visit in northern part of Tanzania to observe Mount Meru, Kilimanjaro, Serengeti, Manyara, Tarangire since places were exposed long time ago.

He said that the Lake Zone and Kigoma Region can make good tourism attractions since there are number of natural attrac-

tions found like presence of national parks and forest reserves mentioning Saramba Island, Ifwanda, Kyperwa, Bwiti-gi, Lubendo, Lake Victoria and Kijevu which have variety of wild animals, birds, snakes, crocodiles and other attracting creatures.

"From now there is a good communication network in this area like a large Mwanza Airport, good road transport and marine transport what is needed is to announce these opportunities so that they become well known, this will open investment from the private sector to devote to do business,"

said Prof Mkwinda.

He added that for the country to succeed in tourism sector there is a need to open other areas which were not known previously while having a lot of tourism attractions and Lake Zone is a unique area so the government has a role to play to encourage private sector to join so as to speed up the process.

Mwanza Region Administrative Secretary Mr Christopher Kacha who was a Chairperson of the meeting said that their aim was to work hard to ensure the tourism sector is able to stand in Lake Zone and Kigoma Regions to

enable the nation to collect a lot of revenue.

He said that what is supposed to be done was to open new tourism opportunities by embarking on a big campaign to expose the area to the wide audience through tourism fair and investment forum.

Tourist Officer Mr Wilfred Mwanza said that their plan to hold Tourism Fair and Investment Forum in Lake Zone and Kigoma Region was a good step since the move will attract and promote the tourism sector in the nation while many investors will come in a big number to make an investment.



A tourist displays a Nile Perch caught at Rubondo Island in Lake Victoria that is similarly expected to promote the Lake Zone envisioned more investment

# Wafugaji wakaidi watangaziwa kياما

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewatangazia kياما kipya wafugaji wanaochungia mifugo kwenye mazao ya wakulima kwa makusudi kuwa ataanzisha utaratibu wa mifugo hiyo kuchinjwa na nyama kugawanywa kwenye shule kwa ajili ya wanafunzi.

Chalamila alitangaza kياما hicho mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa katika kata za Kambikatoto na Mafyeke wilayani Chunya kwa ajili ya kukagua mipaka ya Msimu wa Kambikatoto unaokusudiwa kuhifadhiwa na serikali kupitia Wakala wa Huduma za Msimu (TFS).

Akitzungunza na wananchi wa Kata ya Mafyeke baadhi ya wakulima walilalamika kuwa kuna mmoja wa wafugaji amekuwa akichungia mifugo kwenye mazao yao na wakimuuliza anawacharaza ba kora.

Salala Shega, alisema wakulima wengi wameumizwa na mfugaji huyo na kwam-

ba amekuwa akijivunia utajiri alionao kuwa hata wakimshtaki hatafungwa yeye bali zitafungwa fedha zake.

Alisema wakulima wa eneo hilo hawana raha kutokana na mfugaji huyo ambaye amekuwa akishirikiana na vijana wake kufanya unyama huo dhidi yao.

Baada ya maelezo ya mkulima huyo pamoja na wenzake, Chalamila alitangaza Jeshi la Polisi kumkamata mfugaji huyo mara moja na kumsweka ndani kisha hatua za kumfikisha mahakamani zifuatwe.

Alisema mkulima huyo ni miongoni mwa watu wachache ambao wanaendeleza migogoro na wakulima isiyokuwa na ulazima, na kwamba lugha anayotumia inaashiria kuwa kuna baadhi ya viongozi wanaweza wakawa wanapokea rushwa.

Aliwataka wafugaji hao kuacha tabia hizo kwa maelezo kuwa wao na wakulima wanategemeana katika maisha kwa vile wakulima wanahitaji nyama na maziwa kutoka kwao na wao wanahitaji chakula kutoka kwa wakulima.

Alisisitiza vitendo hivyo vya kuingiza

mifugo kwa makusudi kwenye mazao kikiendelea ataanza kutekeleza utaratibu wa mifugo hiyo kutaifishwa na kuchinjwa kwa ajili ya wanafunzi wa shule mbalimbali mkoani humo.

"Kwenye hili sitani, mimi huwa natoa onyo mara ya kwanza, mara ya pili na ya tatu kisha naanza utekelezaji, sasa nikichinja ng'ombe wenu 10 ndipo mtajua kuwa sitani," alisema Chalamila.

Baada ya maagizo hayo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema mfugaji huyo amekamatwa na yupo katika kituo kidogo cha polisi tayari kwa kusafirishwa kwenda Chunya Mjini.

Alisema lugha anayotumia mfugaji huyo kwa wenzake zinafichafua Jeshi la Polisi na serikali kwa kuhisiwa kuwa kuna vishiri vya rushwa miongoni mwa watendaji wa serikali na polisi.

Alisema mtu huyo atafikishiwa mahakamani na baada ya kesi yake kuisha atafute eneo lingine nje ya Mkoa wa Mbeya la kwenda kufanya shughuli zake za ufugaji.

